

## MNYAMA WA UDH-HIYAH ANAYEFEE KUCHINJWA

يشترط للأضحية ستة شروط: أحدها: أن تكون من بهيمة الأنعام وهي الإبل والبقر والغنم ضأنها ومعزها لقوله تعالى: {وَلِكُلِّ أُمَّةٍ جَعَلْنَا مَنْسَكًا لِيَذْكُرُوا اسْمَ اللَّهِ عَلَىٰ مَا رَزَقَهُمْ مِّنْ بَيْمَتِهِ الْأَنْعَامِ فَإِنَّهَا لِلَّهِ وَمَا رَزَقَهُمْ إِلَّا نَسِيئَةٌ يَوْمَ الْقِيَامَةِ وَالضَّانُّ لِلذَّيْئِ وَالْأَنْعَامُ لِلْغَنَمِ} وبهيمته الأنعام هي الإبل، والبقر، والغنم هذا هو المعروف عند العرب، وقاله الحسن وقتادة وغير واحد. الثاني: أن تبلغ السن المحدود شرعاً بأن تكون جذعة من الضأن، أو ثنية من غيره لقوله صلى الله عليه وسلم: «لا تدبجوا إلا مسنة إلا أن تعسر عليكم فتدبجوا جذعة من الضأن». «رواه مسلم». والمسنة: الثنية فما فوقها، والجذعة ما دون ذلك. والثني من الإبل: ما تم له خمس سنين، والثني من البقر: ما تم له سنتان. والثني من الغنم ما تم له سنة، والجذع: ما تم له نصف سنة، فلا تصح التضحية بما دون الثني من الإبل والبقر والمعز، ولا بما دون الجذع من الضأن. الثالث: أن تكون خالية من العيوب المانعة من الإجزاء وهي: أربعة: 1. العور البين: وهو الذي تنخسف به العين، أو تبرز حتى تكون كالنور، أو تبيض ايضاضاً يدل دلالة بينة على عورها. 2. المرض البين: وهو الذي تظهر أعراضه على البهيمه كالحمي التي تقعد عنها المرعى وتمنع شهيتها، والجرب الظاهر المفسد للحمها أو المؤثر في صحتها، والجرح العميق المؤثر عليها في صحتها ونحوه. 3. العرج البين: وهو الذي يمنع البهيمه من مسايرة السليمه في ممشاها. 4. الهزال المزيل للمخ: لقول النبي صلى الله عليه وسلم حين سئل ماذا يتقي من الضحايا فأشار بيده وقال: «أربعا: العرجاء البين ضلعها، والعوراء البين عورها، والمريضة البين مرضها، والعجفاء التي لا تنقي». «رواه مالك في الموطأ من حديث البراء بن عازب، وفي رواية في السنن عنه ﷺ قال: قام فينا رسول الله صلى الله عليه وسلم فقال: «أربع لا تجوز في الأضاحي» وذكر نحوه. فهذه العيوب الأربعة مانعة من إجزاء الأضحية بما تعيب بما، ويلحق بما كان مثلها أو أشد، فلا تجزى الأضحية بما يأتي: 1. العمياء التي لا تبصر بعينها. 2. المشبومة حتى تثلث وتزول عنها الخطر. 3. المتولدة إذا تعسرت ولادتها حتى يزول عنها الخطر. 4. المصاب بما يميته من خنق وسقوط من علو ونحوه حتى يزول عنها الخطر. 5. الرمى وهي العاجزة عن المشي لعاهة. 6. مقطوعة إحدى اليدين أو الرجلين. فإذا ضمنت ذلك إلى العيوب الأربعة المنصوص عليها صار ما لا يضحى به عشرة. هذه الستة وما تعيب بالعيوب الأربعة السابقة. الشرط الرابع: أن تكون ملكاً للمضحى، أو مأذوناً له فيها من قبل الشرع، أو من قبل المالك فلا تصح التضحية بما لا يملكه كالمغصوب والمسروق والمأخوذ بدعوى باطلة ونحوه؛ لأنه لا يصح التقرب إلى الله بمعصيته. وتصح تضحية ولي البيتيم له من ماله إذا جرت به العادة وكان ينكسر قلبه بعدم الأضحية. وتصح تضحية الوكيل من مال موكله بإذنه. الشرط الخامس: أن لا يتعلق بما حق للغير فلا تصح التضحية بالمرهون. الشرط السادس: أن يضحى بما في الوقت المحدود شرعاً وهو من بعد صلاة العيد يوم النحر إلى غروب الشمس من آخر يوم من أيام التشريق وهو اليوم الثالث عشر من ذي الحجة، فتكون أيام الذبح أربعة: يوم العيد بعد الصلاة، وثلاثة أيام بعده، فمن ذبح قبل فراغ صلاة العيد، أو بعد غروب الشمس يوم الثالث عشر لم تصح أضحيته.....

المصدر: مختصر أحكام الأضحية والذكاة للعثيمين

Yamewekwa masharti sita kwa ajili ya Mnyama wa Udh-hiya:

Sharti la kwanza: **Mnyama wa Udh-hiya awe miongoni mwa wanyama-hoa; nao ni Ngamia na Ng'ombe na Mbuzi na Kondoo** kwa kauli ya Allah Mtukufu: [[ Na kila umma tuliupatia ibada ya kuchinja ili wamtaje Allah kwa sababu ya kuruzukiwa wanyama-hoa ...]] na wanyama-hoa (waliotajwa katika aya hii) ni Ngamia na Ng'ombe na Mbuzi na Kondoo na hivi ndivyo ifahamikavyo kwa waarabu kama alivyotaja Alhassan na Qataadah na wengineo, Allah Awarehemu.

Sharti la pili: **Mnyama awe amefika umri uliopangwa kisheria;**

	Wanyama-hoa	Umri uliopangwa kisheria
1	Ngamia	Miaka 5 au zaidi
2	Ng'ombe	Miaka 2 au zaidi
3	Mbuzi	Mwaka 1 au zaidi
4	Kondoo	Miezi 6 au zaidi

Uchinjaji wa mnyama wa Udh-hiya hautokuwa sahihi endapo amechinjwa Ngamia chini ya miaka mitano, na Ng'ombe chini ya miaka miwili, na Mbuzi chini ya mwaka mmoja na Kondoo chini ya miezi sita.

Sharti la tatu: **Mnyama asiwe na dosari zenye kuzuia ufaaji wake. Na dosari hizo ni nne:**

#### Dosari ya kwanza

Mwenye ubovu wa macho ulio wazi (chongo) naye ni yule ambaye macho yake yamedidimia au yamekodoka mithili ya duara-dufu, au yana weupe kwa ndani ambao unajulisha wazi chongo yake.

#### Dosari ya Pili:

Maradhi yaliyowazi: Nayo ni yale ambayo dalili zake zinadhiri wazi kama vile homa ambayo inamzuia mnyama kwenda malishoni na inamzuia kutamani kula malisho. Au ukurutu mwilini uliodhahiri wenye kuharibu nyama yake au afya yake au jeraha kubwa lenye kuathiri afya yake na mfano wa hayo.

#### Dosari ya Nne

Mnyama dhaifu asiyekuwa na mnofu.

#### Dosari ya Tatu

Mwenye ubovu wa miguu ulio wazi (kiguru/kilema). Nao ni ule ambao unamzuia mnyama kutembea salama anaposwagwa

Kwa kauli ya Mtume swallallaahu alaihi wasallam pindi alipoulizwa ni wanyama gani waepukwe katika udh-hiya, akaashiria kwa vidole vyake kuwa ni wanne kisha akasema: ((Kiguru ulio wazi ulemavu wake, na chongo iliyowazi chongo yake, na mgonjwa ulio wazi ugonjwa wake na mnyama dhaifu asiyekuwa na mnofu ))

Hizi dosari nne zinazuia ufaaji wa mnyama wa Udh-hiyah mwenye dosari hizo. Na dosari nyingine zinazofanana na hizo au zilizokuwa zaidi ya hizo, pia zinaambatana na hizo nne; hivyo basi haifai kuchinja mnyama wa Udh-hiya mwenye dosari zifuatazo:

- 1) Mnyama kipofu asiyeona kabisa kwa macho yake.
- 2) Mnyama aliyevimbiwa sana kisha akaendesha (akaharisha) sana mpaka akatokwa na fahamu.
- 3) Mnyama mwenye kujifungua kwa tabu na ugumu mno mpaka akatokwa na ufahamu.
- 4) Mnyama aliyepatwa na tukio hatarishi kama vile kuzama majini au kuanguka kutoka juu, na mfano wake mpaka akatokwa na ufahamu.
- 5) Mlemavu wa kudumu, naye ni mnyama ambaye anashindwa kabisa kutembea kwa sababu ya ulemavu.
- 6) Mnyama aliyekatwa (au aliyevunjika) mkono mmoja au mguu mmoja.

Ukiongeza dosari hizi sita pamoja na zile nne ambazo zimeelezwa katika hadithi, wanakuwa wanyama wasiofaa kuchinjwa ni kumi; hawa sita na wale wenye dosari zile nne.

Sharti la nne: **Mnyama awe anamilikiwa na mchinjaji au mchinjaji awe kapewa idhini ya kisheria**, au awe kapewa idhini na mmiliki wa mnyama. Haifai kuchinja mnyama wa Udh-hiya asiye kuwa mmiliki wa mchinjaji kama vile mnyama aliyeporwa au kuibwa au aliyepatikana kwa madai ya

uongo, na mfano wa hayo. Kwa sababu haifai kufanya ibada ya kujisogeza kwa Allah kwa njia ya kumuasi Allah. Na inafaa msimamizi wa mali ya yatima kumchinja katika mali yake endapo itakuwa ni kawaida iliyozeleka (katika eneo husika) na ukawa moyo wa yatima unasononeka kwa kutochinja Udh-hiya. Na pia inafaa mwakilishi kuchinja katika mali ya aliyempa uwakala endapo atampa idhini.

Sharti la Tano: **Mnyama wa Udh-hiya asiwe anaambatana na haki ya mtu mwingine**, hivyo haifai kuchinja mnyama ambaye amewekwa rehani.

Sharti la sita: **Achinje mnyama wa Udh-hiya ndani ya wakati uliopangwa kisheria**, nao ni baada ya kumalizika swala ya Eid ndani ya siku ya 10 Dhul-hijjah mpaka lizamapo jua siku ya mwisho katika masiku ya kukausha nyama, nayo ni siku ya tarehe 13 Dhul-hijjah. Hivyo basi, **siku za kuchinja ni nne**, nazo ni: siku ya sikukuu baada ya swala (tarehe 10), na masiku matatu baada yake (tarehe 11, 12 na 13)...]]

وصلی اللہ علی محمد وآلہ وصحبہ وسلم

Mkusanyaji na Mkalimani: Ummati Abdallah, Abuu Muhammad